# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

## KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

OFISI YA BUNGE
**DODOMA**
**17 APRILI, 2020**

# YALIYOMO


1.0. UTANGULIZI .... 2

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 .... 3

3.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA 2019/20.. 4

4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021. .... 6

4.1. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo .... 6

4.2. Maduhuli .... 7

5.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI .... 8

5.1. Changamoto ya Uhaba wa Watumishi .... 8

5.2. Changamoto ya Watumishi wenye maadili .... 8

5.3. Posho za Wazee wa Mabaraza ya Mahakama .... 9

5.4. Mabaraza ya Usuluhisi .... 9

5.5. Uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA .... 10

5.6. Utolewaji wa Fedha za Maendeleo .... 10

5.7. Changamoto ya Miundombinu ya Mahakama za Wilaya Mwanzo na Kata..... 11

6.0. HITIMISHO .... 12

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

## 1.0. UTANGULIZI.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 9(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011 kifungu cha 59, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ni kutafsiri Sheria na kutolea maamuzi kesi mbalimbali zinazoletwa Mahakamani. kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 107(A)(1) Mahakama imepewa mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama hadi Februari, 2020, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishiwa na Bunge jumla ya kiasi cha **Sh. 126,162,464,756.** Kati ya fedha hizo **Sh. 50,145,970,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mahakama (PE), **Sh. 2,377,212,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Sh. 51,481,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh. 22,157,900,756** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, **Sh. 15,000,0000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 7,157,900,756** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 80,689,372,935** ambazo ni sawa na **asilimia 63.9** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo **Sh. 39,130,875,169** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Sh. 32,664,474,980** kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, **Sh. 1,224,864,000** kwa ajili ya Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **Sh. 10,437,010,014** ni fedha za maendeleo kati ya hizo **Sh. 5,161,158,786** ni fedha ndani na **Sh. 2,508,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2019/2020 ulipanga kukusanya maduhuli ya **Sh. 12,328,200,862** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 kiasi kilichokuwa kimekusanywa ni **Sh. 8,004,020,000** ikiwa ni sawa na **asilimia 63.6** ya lengo la mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa utekelezaji wa bajeti hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ni wa kuridhisha isipokuwa kwa fedha za maendeleo za ndani na nje ambazo zimetolewa kwa **asilimia 34.1.** Aidha, fedha hizi zililengwa kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama. Hivyo, kwa mwenendo huu ni wazi kuwa Mahakama haikuweza kutekeleza vipaumbele vyake

kwa ukamilifu na hivyo kufifisha jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi. Kwa mantiki hii, Kamati inaendelea kusisitizia Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kuwa fedha za Mfuko wa Mahakama zinatolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya Mfuko huku ikizingatia maeneo yote ya vipaumbele vya Mfuko.

## 3.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki ilijiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuharakisha usikilizaji wa mashauri, kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kujenga miundombinu na kuongeza matumizi ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezezaji wa Bajeti ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mahakama imefanikiwa kutekeleza vipaumbele vyake kama ifuatavyo:-

a) Kumaliza mashauri 271,214 kati ya mashauri 340,137 yaliyokuwepo mwaka 2019 na hivyo kubakia na mashauri 68,923 mwishoni mwa mwezi Desemba, 2019;

b) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;

c) Kuboresha mfumo wa usajili wa mashauri (Judiciary statistics dashboard system);

d) Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama Kuu za Kigoma na Mara, Ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Manyara, Simiyu, Geita na Njombe na za Wilaya za Longido, Kondoa, Kasulu, Chunya, Bukombe, Chato, Kilwa na Ruangwa. Vilevile, Mahakama za mwanzo za Mkunya

(Newala), Magoma (Korogwe), Msanzina Mtowisa (Sumbawanga), Uyole (Mbeya) na Mlowo (Mbozi) zimekamilika;

e) Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Katavi na Lindi na za Wilaya za Kilindi, Sikonge, Rungwe, Bunda, Makete na Wanging'ombe na Mahakama za mwanzo za Mtae (Lushoto), Ngerengere, Mlimba na Mangu'la (Mororgoro); Laele (Sumbawanga) na Lugawala (Ludewa); na

f) Kuanzishwa kwa Mahakama za Wilaya za Kilindi, Kibiti na Mvomero, ambazo awali zilikuwa zinapata huduma kutoka Wilaya za jirani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Mahakama ilikabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2019/2020:-

i. Upungufu wa watumishi kwa kada mbalimbali ikilinganishwa na mahitaji;

ii. Uhaba wa vitendea kazi, hususan magari kwa ajili ya ukaguzi;

iii. Uhaba wa watumishi wenye sifa na maadili kwa kada mbalimbali; na

iv. Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji na mazingira ya kazi ukilinganisha na unyeti wa kazi ya utoaji haki.

**Mheshimiwa Spika,** aidha changamoto hizi zinazoikabili Mahakama zimekuwepo muda mrefu na zimekuwa zikiripotiwa kila mara. Hivyo, wakati umefika sasa changamoto hizi zikachukuliwa kwa uzito wake na kuweza kutatatuliwa ili Mahakama iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

## 4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kutekeleza malengo ya mpango mkakati waliojiwekea. Aidha, katika mwaka 2020/2021, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo: -

a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (backlog);

b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;

c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

e) Kuanza kwa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuihamishia Dodoma; na

f) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

### 4.1. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya **Sh. 158,437,977,000** ikiwa ni ongezeko la asilimia **25.68** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/20. Kati ya fedha hizo; **Sh. 50,543,824,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mahakama, **Sh. 2,264,771,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, **Sh.**

**53,754,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na **Sh. 51,875,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho **Sh. 39,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 12,875,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** ukomo huu umeongezeka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/2020, hususan eneo la bajeti ya maendeleo. Nyongeza ya bajeti ya maendeleo ya fedha za ndani ni mahsusi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama Dodoma. Aidha, kati ya fedha hizo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ambao utaelekezwa katika kuboresha miundombinu ya Mahakama ikiwa ni pamoja ujenzi wa Mahakama Kuu, Mahakama za Mwanzo na za Wilaya. Ni matumaini ya Kamati kuwa ikiwa fedha hizo zitatoka kama inavyotarajiwa basi Mahakama itaondokana na changamoto ya uhaba ya miundombinu muhimu na hivyo kuleta karibu huduma za Mahakama kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi mengineyo, kuna nyongeza ya **sh. 2,273,000,000** ambazo ni mahsusi kwa ajili ya kugharamia mashauri yanayotokana na Uchaguzi Mkuu, kwa upande wa wabunge na madiwani, mashauri ambayo yana utaratibu maalum wa kuyashughulikia. Kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili, Serikali iliona umuhimu na haja ya kuiongezea Mahakama kiasi hicho cha fedha kwenye bajeti. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa suala hili na kulitengea fedha ili kuhakikisha kuwa mashauri ya namna hiyo yatakapojitokeza yanasikilizwa na kumalizwa kwa wakati.

### 4.2. Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.**

**14,571,199,235** ikiwa ni ongezeko la **Sh. 2,000,000,000** ikilinganishwa na makadirio ya **Sh. 12,571,199,235** ya mwaka 2019/2020.

## 5.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1. Changamoto ya Uhaba wa Watumishi

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali hususani Majaji, Mahakimu na Makarani. Aidha, changamoto hii imekuwa ya muda mrefu na kusababisha Mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwa awamu kwenye kada mbalimbali kulingana na maombi yaliyowasilishwa ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mahakama. Hatua hii iende sambamba na uongezwaji wa mishahara na maslahi ya watumishi ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

### 5.2. Changamoto ya Watumishi wenye maadili

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama imekuwa na changamoto ya maadili kwa baadhi ya watumishi wa Mahakama. Na kwa kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ndio yenye jukumu la kushughulika na maadili ya watumishi, Kamati inasisitizia Tume ya Utumishi kuwatambua na kuwachukulia hatua watumishi ambao wanaenda kinyume na maadili ya utumishi wa Mahakama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba utaratibu uliowekwa kisheria wa Kamati ya Maadili ya Wilaya chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya umekuwa haufanyiki kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Kamati hii ya maadili ndiyo inahusika na kusikiliza tuhuma za uvunjifu wa maadili wa watumishi wa mahakama katika ngazi ya Wilaya na kuwachukulia hatua. Hivyo ni wazi kwamba bila kutenga

rasilimali fedha za kuwezesha vikao hivi kufanyika kikamilifu tatizo la maadili kwa watumishi wa Mahakama litaendelea kuwepo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha ili vikao vya Kamati ya Maadili vifanyike kama sheria inavyotaka.

## 5.3. Posho za Wazee wa Mabaraza ya Mahakama

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeze posho zinazolipwa kwa wazee wa mabaraza ya Mahakama. Wazee wa mabaraza wanalipwa kiasi cha sh. 5,000 kwa kila kesi kiasi, ambacho Kamati inaona ni kidogo lakini vivle vile kimekuwa hakilipwi kwa wakati na hivyo kusababisha madeni. Wazee hawa kuendelea kudai posho zao kunawaondolea heshma na kuweka mazingira ya kuhitaji rushwa kutoka kwa watuhumiwa. Hivyo, wakati Serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza kiwango hicho iangalie uwezekano wa kuhakikisha kuwa posho hizo zinalipwa kwa wakati na hakuna malimbikizo ya madeni.

## 5.4. Mabaraza ya Usuluhisi

**Mheshimiwa Spika,** mabaraza ya usuluhishi yalianzishwa kwa Sheria namba 5 ya mwaka wa 1985 kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mahakama lakini mabaraza haya badala yake yamekuwa ya kiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutokana na kutawala kwa rushwa na kutokuwa na uelewa wa masuala ya utoaji haki. Aidha, mabaraza haya yanasimamiwa na kamati ya maendeleo ya kata na miongoni mwa kanuni za baraza ni baraza kuundwa na wananchi wa kawaida tu wasio na uelewa wa sheria suala ambalo linapelekea haki kutotolewa kwa usawa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hii Kamati kwanza inaona haja ya kurejea na kupitia upya sheria iliyoanzisha mabaraza ya usuluhishi kwenye ngazi ya chini ili kubadili mfumo huu wa mahakama ikizingatiwa sharia hiyo ni ya muda mrefu. Aidha, mabadiliko haya yanatakiwa kuwa na mawanda mapana zaidi kwa mabaraza mengine yanayotumika kutoa haki mathalani mabaraza ya ardhi ili kuleta haki na usawa kwa wananchi. Pili, Serikali iimarishe usimamizi wa mabaraza husika kwani imebainika kuwa mabaraza haya hayana usimamizi mzuri na mengine kutokukaguliwa na kufuatiliwa utendaji kazi wake na mwisho Serikali kuhakikisha kuwa uteuzi wa mabaraza yaliyopo yalizingatia Sheria iliyozianzisha.

## 5.5. Uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** bado Mahakama ina uhaba mkubwa wa vitendea kazi hasa vitendea kazi vya TEHAMA kwa upande wa vifaa vya kurekodi wa mashauri ya vikao ambao unafanywa kwa kuandika kwa mkono. Majaji kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakiandika mashauri kwa mkono suala ambalo haliendani na hali halisi ya kidigitali iliyopo sasa. Aidha, njia hii pia inachukua muda mrefu na hivyo kupelekea Mahakama kushindwa kuwa shindani na kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Hivyo ni vema Mahakama ikaanzisha programu ya mifumo ya kurekodi mashauri haraka iwezekanavyo.

## 5.6. Utolewaji wa Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama inategemea kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia ambao utaenda kutekeleza mpango wa maendeleo wa miiundombinu ya Mahakama. Kupitia mkopo huo Mahakama inatarajia kukamilisha ujenzi wa mahakama za wilaya

33 na mahakama kuu 6. Kamati inasisitiza Serikali kushirikiana na Mahakama katika utolewaji wa fedha hizo ili hatimaye kuwepo na mazingira mazuri ya kutolea haki katika kila pande za nchi.

### 5.7. Changamoto ya Miundombinu ya Mahakama za Wilaya, za Mwanzo na Kata.

**Mheshimiwa Spika,** kuna changamoto kubwa ya uhaba wa miundombinu ya Mahakama za mwanzo katika ngazi za tarafa na kata na wakati mwingine Mahakama hulazimika kukodi majengo ya watu binafsi ili kuendesha mashtaka. Hali hii si nzuri sana kwa chombo kama Mahakama kwa sababu Mahakama inaweza ikashawishika kwenda kinyume na misingi ya utolewaji wa haki mathalani pale inapotokea mwenye jengo ndio amepelekwa mahakamani. Aidha, uhaba wa mahakama hizo umesababisha adha kubwa kwa Wananchi nakuongeza gharama za kufuatilia mashauri hayo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza Mpango Mkakati wa Mahakama wa kujenga miundombinu ya Mahakama katika ngazi za tarafa na kata ili kuondoa adha kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Katiba na Sheria na Mahakama kwa mahusiano mazuri ambayo yanajengwa baina yao. Kamati inakiri kuwa haikuwa na wakati mgumu wa kupitisha bajeti ya Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2020/21 ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo kulikuwa na mivutano baina ya Taasisi hizi. Hivyo, Kamati inasisitiza mahusiano haya mazuri ambayo yanaonekana kuendelea na hatimaye kuleta tija katika ujenzi wa Taifa.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Ndg. Mathias Kabunduguru Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – M/Mwenyekiti
2) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
3) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
4) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
5) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
6) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
7) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
8) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
9) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
10) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
11) Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
12) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb

13) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb

14) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb

15) Mhe. Hasna Sadi Katunda Mwilima, Mb

16) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb

17) Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb

18) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb

19) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb

20) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb

21) Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb

22) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb

23) Mhe. John Kibera Kishimba, Mb

24) Mhe. Andrew John Chenge, Mb

25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb

26) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb

27) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

Mashimba M. Ndaki, Mb

**M/MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

17 Aprili, 2020